# EWC III

## Mkutano wa Tatu wa Kimataifa juu ya Onyo la Awali

*Kutoka Wazo hadi Utekelezaji*

27 29 Machi 2006
Bonn, Germany

# Kuimarisha Taratibu za Onyo la Awali: Uhakiki

International Strategy ISDR for Disaster Reduction

Federal Foreign Office

# UTANGULIZI

Hadhari ni kipengele muhimu katika kupunguza athari za maafa. Huzuia upotevu wa maisha na kupunguza athari za kiuchumi na vitu katika Maafa. Ili iweze kufaa, taratibu zote za hadhari zapasa kushirikisha jamii yote iliyoko kwenye hatari, kutoa elimu na ufahamu wa hatari ya maafa, upashanaji thabiti wa habari na hadhari na kuhakikisha kuna hali ya kuwa tayari kila mara.

Mwezi Januari 2005, Mkutano wa Dunia juu ya kupunguza Maafa ulipitisha "Mpango wa Hyogo wa Utekelezaji wa mwaka 2005-2015: Kujenga ufahamu wa Mataifa na Jamii juu ya Maafa". Hii ilikuwa ni pamoja na umuhimu wa kuwepo hadhari, na ulihimiza uimarishaji *"taratibu za hadhari ambazo zitawashirikisha watu wenyewe, hasa taratibu ambazo hadhari yake ni ya wakati unaofaa na kueleweka kwa wale wanaohusika (…) pamoja na jinsi watu watakavyofanya wakihadharishwa (…)"* (para. 17, ii.d.9).

Mkutano wa Tatu wa Kimataifa juu ya Hadhari (EWC III) uliofanyika mjini Bonn, Ujerumani kutoka tarehe 27-29 Machi 2006 ulitoa nafasi ya kuwasilisha miradi mipya ya ubunifu na kujadilia maafa ya kiasili na hatari zake kote duniani na jinsi athari zake zinavyoweza kupunguzwa kupitia utekelezaji wa utaratibu wa hadhari unaowashirikisha watu. Kijitabu hiki "Kuimarisha Taratibu za Hadhari: Orodha ya Uhakiki" kilitayarishwa kama matokeo ya mkutano, ili kiweze kufahamisha na kuonyesha mijadala pamoja na mifano ya utekelezaji iliyojitokeza katika mkutano huo, na pia kuunga mkono utekelezaji wa vipengele vyote vya Mpango wa Utekelezaji wa Hyogo.

Orodha ya Uhakiki ambayo imejengwa katika mtazamo wa viegezo vyote vinne vya taratibu za hadhari, ina shabaha ya kuwa orodha ya kawaida ya vipengele muhimu na hatua ambazo serikali za mataifa au mashirika ya kijamii yataweza kufanya marejeo wakati wa kuandaa na kutathmini taratibu za hadhari au hata kwa kuangalia tu kwamba taratibu muhimu zimewekwa. Haikusudiwi kuwa itakuwa mwongozo wenye kila kitu lakini badala yake ni chombo cha rejea kisichokuwa-cha kiufundi, bali cha kuhakikisha kunakuwepo utaratibu mzuri wa hadhari.

## Shukrani


Orodha hii ya Uhakiki ilizinduliwa na Sekretarieti ya Mkutano wa Tatu wa Kimataifa juu ya Hadhari kwa ufadhili kutoka kwa Serikali ya Ujerumani. Mradi huu uliongozwa na Mshauri Alison Wiltshire, katika Jukwaa la ISDR la Kuimarisha Onyo la Awali (PPEW) mjini Bonn. Pamoja na habari zilizokuswanywa kwa muda wa siku mbili na nusu za mkutano huo, michango yenye manufaa ilipokelewa kutoka kwa mashirika pamoja na watu binafsi walioshiriki katika upunguzaji wa maafa kwa njia ya hadhari na hatari ya kupatwa na maafa katika utaratibu wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa na kwingineko.

Hisani na shukrani ziende kwa wote waliochangia katika zoezi hili la pamoja, ikiwa ni pamoja na washiriki na wawasilishaji wa mradi huu wa Mkutano wa Tatu wa Kimataifa juu ya hadhari ambao walitoa mawazo yao kwa uwazi, wasiwasi walionao na uzoefu wao wa utendaji juu ya jinsi tutakavyofikia ufanisi wa taratibu za hadhari zinazowaweka watu katika upeo wao.


> *"Nchi zitakazoendeleza sheria za usimamizi na taasisi juu ya kupunguza athari za maafa na kuwa na uwezo wa kuimarisha na kufuatilia kupitia mipango thabiti, zitakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kukabiliana na hatari na kupata kutambuliwa vilivyo kwa kujiingiza na kukabiliana na upunguzaji hatari za maafa miongoni mwa sekta zote za kijamii."*
>
> Mpango wa Utekelezaji wa Hyogo kwa 2005-2015: Unajenga Ukakamavu wa kukabiliana na Maafa ya Mataifa na Jamii. Kifungu 16.

# YALIYOMO

Kijitabu hiki kina shabaha ya kuwasilisha uhakiki mfupi na rahisi wa vipengee vya msingi, utekelezaji na uadilifu unaohusiana na taratibu bora za hadhari. Inakusudiwa kwamba haitakuwa chombo cha kiufundi mbali na kuwa orodha ndefu ya 'jinsi ya" kwa mfumo wa taratibu za hadhari.

## Jinsi ya Kutumia Uhakiki

Kijitabu hiki kimegawanyika katika sehemu mbili zinazoshabihiana ambazo yapasa zisomwe kwa mpangilio. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo muhimu ya kimsingi na maswala dhahiri juu hadhari. Sehemu ya pili ni msululu wa hatua za uhakiki na mawaidha yanayopasa kuzingatiwa wakati wa kuimarisha au hata kutathmini taratibu za hadhari.

***1. Vipengele muhimu vya hadhari, maswala nyeti na wahusika katika hadhari***

Sehemu ya muhtasari juu ya vipengee vinne vya hadhari: Ufahamu wa athari; ufuatiliaji wa kiufundi na huduma ya hadhari; mawasiliano na utoaji wa hadhari; na uwezekano wa jamii kuhusika umejumuishwa kwa ajili ya kutilia mkazo vipengele muhimu zaidi ambavyo ni muhimu kwa kuwashirikisha watu katika utaratibu wa hadhari, na ni kwa nini kila kimoja ni muhimu.

Pamoja na vipengele hivyo vinne, maswala kadhaa yaliyo nyeti ambayo ni muhimu kwa uimarishaji wa uendelevu wa taratibu kabambe za hadhari zimeelezwa. Hizi ni pamoja na usimamizi mzuri na mipango ya taasisi, mtazamo wa athari nyingi kwa hadhari, kuihusisha jamii na kuhakikisha kuna mtazamo wa kijinsia na kitamaduni.

Maelezo juu ya wahusika muhimu katika shughuli za hadhari, na majukumu na wajibu wao, yamejumuishwa kwa sababu ya kutilia uzito pamoja na maelezo ya kimsingi kwa orodha ya wahusika muhimu wanaojulishwa mwanzoni mwa kila orodha ya uhakiki.

***2. Orodha ya uhakiki wa matukio ya utekelezaji ili kusaidia katika, kuimarisha, kutathmini na kurekebisha kabisa utaratibu wa hadhari***

Kwa kurahisisha matumizi na utendaji, orodha binafsi ya uhakiki imetolewa kwa kila moja ya vipengele vyote vinne vya hadhari. Orodha nyingine ya ziada ya uhakiki pia imetayarishwa juu ya maswala nyeti ya usimamizi na mipango ya taasisi kutokana na umuhimu wa swala hili kuwa endelevu na uhamasishaji wa taratibu zinazofaa za hadhari.

Kila moja ya orodha hizi za uhakiki imewekwa chini ya msululu wa makundi ya wito maalumu na inajumuisha orodha ya kawaida ya vitendo au hatua ambazo ikiwa zitazingatiwa, zitatoa msingi thabiti wa kujenga au kukadiria utaratibu wa hadhari.

> *"Mambo mengi yamekuwa funzo kutokana na juhudi za ubunifu za kuzuia maafa za jamii maskini katika nchi zinazoendelea. Sera ya uzuiaji ni muhimu mno kuachiwa serikali na mashirika ya kimataifa wenyewe. Ili kufaulu lazima ishirikishe pia jamii ya wasomi, sekta binafsi na vyombo vya habari."*
>
> Kofi Annan
>
> Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa
>
> Mkutano wa Mpango wa Kimataifa wa Mwongo wa kupunguza maafa ya kiasili (IDNDR)
>
> Geneva, Julai 1999

# TARATIBU ZA HADHARI ZINAZOSHIRIKISHA WATU

## 1. Vipengele Vilivyo Muhimu

Shabaha ya taratibu za hadhari zinazoshirikisha watu ni kuwawezesha watu binafsi na jamii inayotishiwa na maafa kwa ujumla kuchukua hatua kwa wakati unaofaa na kwa njia inayofaa, ili kupunguza uwezekano wa mtu kujeruhiwa, kupoteza maisha na uharibifu wa mali na mazingira.

Utaratibu wa hadhari uliokamilika na unaofaa una vipengele vinne vinavyo-husiana, kuanzia ufahamu wa maafa na uwezekano wa kuathiriwa hadi utayari na uwezo wa kuitikia. Taratibu bora zaidi za hadhari zinazotumika pia zinaingiliana vilivyo na njia nzuri za mawasiliano kati ya vipengee vyote.

### Ufahamu wa Athari

Athari hutokea katika mchangamano wa majanga na na uwezekano wa kuathiriwa katika eneo maalumu. Ukadiriaji wa hatari huhitaji utaratibu kabambe wa ukusanyaji wa takwimu na lazima uchukulie maanani nguvu ya maafa ya kiasili na uwezekano wa kuathiriwa ambao hutokea kutokana na taratibu kama vile za makazi mijini, mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika sehemu za mashambani, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Ukadiriaji wa hatari na ramani husaidia kuwatia watu motisha, ya kutoa kipaumbele taratibu za hadhari na kuongoza maandalizi ya kuzuia maafa na mwitikio.

### Huduma ya Kufuatilia na Hadhari

Huduma za hadhari zipo katikati ya utaratibu. Lazima kuwepo msingi thabiti wa kisayansi kwa ajili ya kubashiri na kutabiri maafa na utaratibu wa hadhari unaoweza kutegemewa na ambao unatumika saa 24 kwa siku. Kuendelea kufuatilizia vigezo vya maafa na vitangulizi ni muhimu kwa kutoa hadhari sahihi kwa mtindo na kwa wakati unaofaa. Huduma za hadhari kwa maafa mbalimbali yapasa zishirikishwe vilivyo inapowezekana ili kupata manufaa kwa ushirika wa mitandao ya taasisi, taratibu na mawasiliano.




*Vipengee vine vya taratibu za hadhari zinazowashirikisha watu.*

**Chanzo:** Jukwaa la UN/ISDR la kutangaza Hadhari

### Usambazaji na Mawasiliano

Hadhari lazima iwafikie wale walioko katika hatari. Ujumbe ulio wazi na wenye maelezo rahisi, na ya kufaa ni muhimu sana kwa kuwezesha mwitikio mzuri ambao utasaidia kuokoa maisha na mali. Taratibu za mawasiliano za maeneo, kitaifa na kijamii lazima zitambuliwe kwanza na sauti zenye nguvu kuanzishwa. Matumizi ya njia nyingi za mawasiliano ni muhimu kuhakikisha watu wengi iwezekanavyo wanaohadharishwa, ili kuepukana na kushindwa kwa njia yoyote, na kuimarisha ujumbe wa hadhari.

### Uwezo wa Kuitikia

Ni muhimu kwa Jamii kuelewa hatari yao; kuheshimu huduma za hadhari na kufahamu jinsi ya kuitikia. Mipango ya kuelimisha na maandalizi ni muhimu zaidi. Ni muhimu pia kwamba mipango ya usimamizi ikawekwa bayana, kufanyiwa mazoezi na kujaribiwa. Jamii lazima ifahamishwe barabara juu ya chaguo la tabia ya usalama, sehemu za kujiokoa, na jinsi ya kujiepusha na uharibifu na upotevu wa mali.

## 2. Maswala Nyeti Zaidi

Kuna msululu wa maswala nyeti ambayo lazima yatiliwe maanani wakati wa kuunda na kudumisha taratibu zinazofaa za hadhari.

**Utawala Bora zaidi na Mipango ya Kitaasisi**

Utawala bora ulioimarika na mipango ya kitaasisi huchangia vyema ufanisi wa uimarishaji na uendelevu wa taratibu kabambe za hadhari. Ni msingi unaobeba vile vipengele vinne vilivyotajwa hapo mwanzo vya hadhari kwa kujenga, kuimarisha na kudumisha.

Utawala bora unahimizwa na sheria na mitindo ya usimamizi na kuungwa mkono na mipango ya uwajibikaji wa kisiasa wa muda mrefu pamoja na mipango ya taasisi inayotumika. Mipango ya usimamizi mzuri yapasa ihimize utoaji maamuzi na ushiriki ambavyo vinachukuliwa na uwezo mpana zaidi wa usimamizi katika kiwango cha kitaifa na kimaeneo.

Mawasiliano ya juu na ya chini pamoja na ushirikishwaji wa wahusika wa hadhari lazima pia kuanzishwa.

**Mtazamo Mseto wa Majanga**

Inapowezekana, mfumo wa hadhari uunganishe mtazamo wa mfumo wa majanga yote Viwango vya uchumi, uendelevu na ufanisi yaweza kuimarishwa ikiwa taratibu na shughuli za utendaji zimeanzishwa na kudumishwa katika mtazamo wa utaratibu wa matumizi ya njia nyingi ambazo zinazingatia majanga ya aina zote na mahitaji ya mtumiaji wa mwisho.

Hadhari za hatari za aina nyingi pia zitaanzishwa mara kwa mara, kuliko hadhari ya maafa ya aina moja. Na kwa hivyo kuweza kutumika vyema zaidi na kuweza kutegemewa kwa hatari kali zaidi na kubwa kama vile Tsunami ambazo hutokea mara kwa mara. Taratibu hizi za hatari za aina nyingi, pia husaidia watu kufahamu vyema na hatari zinazowakabili na kuimarisha hatua zao za kujiandaa na tabia za kuitikia hadhari.

**Uhusishaji wa Jamii Husika**

Taratibu za hadhari zinazoshirikisha watu hutegemea ushiriki wa moja kwa moja wa wale ambao wako katika tishio la kupatwa na hatari. Bila kushirikisha mamlaka za mitaa na watu wa kawaida, na jamii zilizo katika tishio la kupatwa na hatari, miingiliano ya serikali na taasisi na muitikio kwa matukio ya hatari huenda ukapungua.

Mtazamo mwingine wa hadhari, wa "chini kwenda juu" pamoja na ushirikishi wa jamii huwezesha mwitikio wa aina nyingi kwa matatizo na mahitaji. Kwa njia hii, jamii husika, makundi ya wanaharakati na mipangilio ya kitamaduni vinaweza kuchangia katika hali ya uwezekano wa kuathiriwa, na kuimarishwa kwa uwezo wa jamii.

**Kufikiria Mukhtadha wa Kijinsia na Tofauti za kitamaduni**

Katika kuimarisha taratibu za hadhari ni muhimu kutambua kwamba makundi tofauti yana aina mbalimbali za tishio la hatari kulingana na utamaduni, jinsia au maumbile mengine yoyote yale ambayo yanashawishi uwezo wao wa kushiriki katika kujiandaa, kuzuia na kukabiliana na maafa. Mara nyingi, wanawake na wanaume huwajibika tofauti katika jamii na hupata habari kwa njia mbalimbali zinazotofautiana kuhusu maafa. Pamoja na hayo, wazee, walemavu na wale ambao hawakubahatika kiuchumi mara nyingi huwa katika hatari ya kuathiriwa zaidi.

Habari, mipango ya taasisi na taratibu za utoaji hadhari lazima itayarishwe kulingangana na mahitaji ya kila kundi katika kila jamii iliyoko katika hatari ya kuathiriwa.

# 3. Wahusika Muhimu

Kuimarisha na kutekeleza mpango kabambe wa utaratibu wa hadhari unahitaji mchango na ushirikishaji wa idadi kubwa ya watu binafsi na makundi. Orodha inayofuata inaeleza kwa kifupi aina ya makundi na mashirika yanayopasa kushirikishwa katika taratibu hizi za hadhari na jinsi yanavyofanya kazi na wajibu wao.

**Jamii,** hasa wale ambao wako katika hatari ya kudhuriwa, ndiyo hasa wanaohitaji kushirikishwa katika taratibu za hadhari. Yapasa washiriki kwa kila njia katika utaratibu wote na utekelezaji wa hadhari; wawe na tahadhari juu ya hatari na uwezekano wa athari zilizo mbele yao; na waweze kuchukua hatua ya kupunguza tishio la upotevu au uharibifu.

**Serikali za Mitaa,** Kama vile Jamii na watu binafsi, serikali za mitaa ziko katikati kabisa ya taratibu zifaazo za hadhari. Yapasa zisaidiwe na serikali za taifa, zifahamishwe barabara juu ya hatari za maafa zinazotishia usalama wa watu wao na kushiriki katika kubuni na kutekeleza taratibu za hadhari. Lazima waelewa pia maelezo ya ushauri wanayopokea na kuweza kushauri, kuagiza na kuwashirikisha watu katika mfumo ambao utaongeza usalama wa raia na kupunguza uwezekano wa upotevu wa mali asili inayotegemewa na jamii.

**Serikali za Taifa** Zinawajibika kuwa na sera thabiti na mikakati ambayo inaruhusu utekelezaji wa taratibu za hadhari na taratibu za kiufundi ambazo hubashiri na kutoa ilani za hatari. Serikali za Taifa zinawajibika kuingiliana na serikali za maeneo na za kimataifa na mashirika kwa ajili ya kuiimarisha zaidi uwezo wa hadhari na kuhakikisha kwamba hadhari zinaelekezwa zaidi kwa watu walioko katika tishio la kuathiriwa katika sehemu zote zinazohusika. Utoaji wa msaada kwa jamii na serikali mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa utekelezaji pia ni jambo muhimu.

**Taasisi za Maeneo na Mashirika** Zinachukua jukumu la kutoa elimu ya kipekee na ushauri ambao utasaidia juhudi za taifa za kuimarisha na kuendeleza uwezo wa hadhari katika nchi ambazo zina mazingira sawa ya kijiografia. Pamoja na hayo mashirika haya yanahimiza maingiliano na mashirika ya kimataifa na kuhamasisha njia za hadhari zinazofaa miongoni mwa nchi zinazopakana.

**Mashirika ya Kimataifa** yanaweza kusaidia uratibu wa kimataifa, uwiano na ufadhili kwa shughuli za hadhari ya taifa na pia kutoa nafasi ya ubadilishanaji wa takwimu na ufahamu kati ya nchi mbalimbali na maeneo. Ufadhili waweza kuwa kwa njia ya kutoa maelezo ya ushauri, msaada wa kiufundi, pamoja na sera na maandalizi ya msaada unaotakiwa kusaidia maendeleo na uwezo wa utekelezaji wa mamlaka ya serikali au mashirika.

**Mashirika Yasiyo ya Serikali** huchukua jukumu la kutoa elimu kwa watu binafsi, jamii na mashirika yanayohusika katika hadhari, hasa katika ngazi ya jamii. Yanaweza pia kusaidia katika utekelezaji wa taratibu za hadhari na kuitayarisha jamii kukabiliana na maafa. Pamoja na hayo yanaweza kuchukua jukumu la utetezi wa sheria kusaidia kuhakikisha kwamba taratibu za hadhari zinakuwa ajenda miongoni mwa viongozi wa serikali wanaobuni sera.

**Sekta Binafsi** ina jukumu kubwa zaidi la kutekeleza hadhari , ikiwa ni pamoja na kujenga taratibu za uwezo wa kuwa na hadhari katika mashirika yao. Vyombo vya habari huchukua jukumu muhimu la kuhakikisha kwamba habari za maafa zinajulikana kwa watu wote na pia kwa kusambaza habari za hadhari. Sekta binafsi pia ina uwezo mkubwa ambao haujatumika kusaidia kutoa huduma za kitaalamu, kiufundi, ufahamu, au michango ya (hali na mali) ya bidhaa au huduma.

**Jamii ya Wanasayansi na Wasomi** inawajibika kutoa mchango wake wa kisayansi na kiufundi ili kusaidia serikali na jamii katika kuimarisha taratibu za hadhari**.** Utaalamu wao una umuhimu wa kuchambua tishio hatari la kiasili linalokabili jamii, kufadhili miundo ya kisayansi na kufuatilia huduma za hadhari, kufadhili ubadilishanaji wa takwimu, kutafsiri taarifa ya kisayansi au ya kiufundi hadi kuwa ujumbe wa kawaida na kusambaza hadhari zinazoeleweka kwa wale wnaotishiwa na hatari.

***Kipengele muhimu 1:*** **UFAHAMU WA HATARI**

**Shabaha:** *Kuanzisha utaratibu wenye mpangilio wa kawaida wa kukusanya, kukadiria na kubadilishana takwimu, ramani na mwelekeo wa majanga na uwezekano wa kuathiriwa.*

## Washiriki Muhimu

Mashirika ya usimamizi wa hatari ambayo ni ya Kimataifa, kitaifa na kiwilaya; mashirika ya utabiri wa hali ya hewa na Usimamizi wa maji; wataalamu wa mambo ya kijamii; na wanasayansi; wahandisi; wachoraji ramani za nyumba na mitaa ya miji; na wasomi, mashirika na waakilishi wa Kijamii wanaoshughulika na usimamizi wa hatari za maafa Mashirika ya kimataifa na ya Umoja wa Mataifa kama vile WMO, UN/ISDR, UNEP, UNU-EHS, UNOSAT, UNDP, FAO, UNESCO.

## Orodha ya Uhakiki

**1. Mipango ya Usimamizi iliyowekwa**

- ☐ Mashirika muhimu ya serikali yanayohusika na majanga na ukadiriaji wa uwezekano wa kuathiriwa kutambuliwa na majukumu yao kupambanuliwa (k.m. mashirika yanayoshughulikia takwimu za kiuchumi, takwimu za idadi ya watu, mipango ya matumizi ya ardhi, takwimu za kijamii n.k.).
- ☐ Wajibu wa kuratibu utambuzi wa majanga ukadiriaji wa uwezekano wa kuathiriwa na hatari kupewa shirika moja la taifa.
- ☐ Sheria au maagizo ya maongozi ya serikali ya kutoa idhini ya uandalizi wa hatari na ramani za hofu ya kuathiriwa kwa jamii zote zilizopo.
- ☐ Viwango vya kitaifa kwa ajili ya ukusanyaji wa kimpango, ubadilishanaji wa takwimu za hatari na hofu ya kuathiriwa zilizoimarishwa, na kusawazishwa na zile za nchi au eneo, inapohitajika.
- ☐ Utaratibu wa wataalamu wa kisayansi na kiufundi kwa kukadiria na kuchunguza usahihi wa takwimu ya hatari na kuimarisha taarifa.
- ☐ Mikakati ya kuwashirikisha jamii katika hatari za maeneo yao na uchambuzi wa maeneo yanayokuwa katika hatari ya kuathiriwa.
- ☐ Utaratibu wa uchunguzi na kuandikwa upya takwimu za hatari kila mwaka na kujumuisha mabadiliko ya takwimu juu ya hofu ya kuathiriwa na hatari zilizotokea.

**2. Hatari za kiasili zilizotokea**

- ☐ Tabia ya majanga makuu ya kiasili yaliyotokea (k.m. nguvu, kurudiarudia na matarajio) Uchambuzi na data za kihistoria kutahminiwa.
- ☐ Ramani za hatari kuimarishwa kwa ajili ya kutambua maeneo ya kijiografia na jamii ambazo huenda zikaathiriwa na maafa ya kiasili.
- ☐ Kustawishwa ramani ya mseto (inapo wezekana) kukadiria mwingiliano wa maafa makubwa ya kiasili.

**3. Uchambuzi wa Hatari ya kuathiriwa kwa Jamii**

- ☐ Makisio ya hatari ya kuathiriwa kufanywa kwa kila maafa ya kiasili yaliyoko.
- ☐ Vyanzo vya takwimu za kihistoria na uwezekano wa kuzuka hatari baadaye kufikiriwa katika hatari ya kuathiriwa.
- ☐ Vipengele kama vile jinsia, ulemavu, uwezo wa kufikia miundombinu, utandawazi wa kiuchumi na athari za kimazingira kufikiriwa.
- ☐ Hatari za kuathiriwa kunakiliwa na kuwekwa katika ramani (k.m. watu au jamii wanaoishi maeneo ya pwani kutambuliwa na kuwekwa katika ramani).

**4. Makisio ya Hatari**

- ☐ Miingiliano ya maafa na hatari ya kuathiriwa kukisiwa ili kujua hatari inayokabili kila eneo au jamii.
- ☐ Ushauri wa kijamii na wa sekta ya viwanda huendeshwa ili kuhakikisha maelezo ya usahihi kuhusiana na hatari na yanajumuisha ufahamu wa kihistoria na kiasili, na viwango vya takwimu ya maelezo ya kimaeneo na kitaifa.
- ☐ Shughuli ambazo zinaongeza hatari kutambuliwa na kutathminiwa.
- ☐ Matokeo ya makisio ya hatari kuunganishwa na mipango ya usimamizi wa hatari na ujumbe wa hadhari katika maeneo.

**5. Uhifadhi wa Taarifa na Upatikanaji Wake**

- ☐ Kuanzilisha Maktaba kuu au GIS kwa ajili ya kuhifadhi takwimu na matukio yote ya maafa na hatari za majanga ya kiasili.
- ☐ Takwimu juu ya hatari na uwezekano wa kuathiriwa kufikia serikali, raia na jamii ya kimataifa (kila inapohitajika).
- ☐ Mpango wa utunzaji wa takwimu kubuniwa na kuhakikisha kwamba inarekebishwa kila mara ili iende na wakati.

## *Kipengele muhimu 2:* HUDUMA YA KUFUATILIA NA HADHARI

**Shabaha:** *Kuanzisha huduma inayofanya kazi vizuri ya kufuatilia majanga na kutoa hadhari katika msingi thabiti wa Kisayansi na Kiteknolojia.*

### Washiriki Muhimu

Huduma ya taifa ya Utabiri wa hali ya hewa na Maji; Vituo vya kipekee vya uchunguzi na hadhari; (k.m. kwa maji, Tsunami, Volkeno na hali ya hewa); Vyuo vikuu; taasisi za utafiti; watoaji vifaa katika sekta za kibinafsi; mamlaka za mawasiliano ya simu; wataalamu wa shughuli za usimamizi; vituo vya kiufundi katika maeneo; na Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile UN/ISDR, WMO, FAO, UNESCO, UNEP, UNOSAT, OCHA, ITU.

### Orodha ya Uhakiki

**1. Utaratibu wa Kitaasisi kuanzishwa**

- ☐ Kuleta viwango vya utaratibu, na majukumu na uwajibikaji wa mashirika yote yanayotayarisha na kutoa hadhari zinazobuniwa na kuendeshwa kisheria.
- ☐ Kuanzishwa mikataba na kuunganishwa protokali ili kuhakikisha uendelevu wa lugha ya kutoa hadhari na njia za mawasiliano pale ambapo aina fulani ya hatari inasimamiwa na mashirika tofauti.
- ☐ Mpango wa aina zote za hatari kwa ajili ya kupata utendaji mzuri unaokubalika na uwezo miongoni mwa taratibu mbalimbali za hadhari kuanzishwa.
- ☐ Washiriki wa utaratibu wa hadhari, ikiwa ni pamoja na mabaraza ya miji, ambapo mashirika yanayojulikana yanalazimika kuwajibika kwa hadhari.
- ☐ Kuwekwa protokali ambazo zitaeleza uwajibikaji wa mawasiliano na njia za huduma za hadhari na za kiufundi za hadhari.
- ☐ Mipango ya mawasiliano na mashirika ya kimataifa na ya kimaeneo yaliyokubaliwa na yanayofanya kazi.
- ☐ Mikataba ya kimaeneo, vyombo vya uratibu na vituo maalumu kuwekwa kwa mahitaji ya kimaeneo kama vile vimbunga, mafuriko katika mabonde ya pamoja, ubadilishanaji wa takwimu na uimarishaji wa uwezo wa kiufundi.
- ☐ Taratibu za hadhari ambazo zimefanyiwa majaribio na mazoezi angalau mara moja kwa mwaka.
- ☐ Kamati kuu ya Taifa ya hatari zote juu ya taratibu za hadhari kwa utaalamu ziwekwe na ziunganishwe na Idara ya usimamizi wa Maafa kwa taifa na Mamlaka za Kusimamia Upunguzaji, ikiwa ni pamoja na jukwaa la taifa la kupunguza athari za maafa.
- ☐ Utaratibu uanzilishwe kuhakikisha kwamba hadhari inawafikia watu walio kusudiwa.
- ☐ Vituo vya hadhari viwe na wafanyakazi kila mara (saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki).

**2. Kuimarishwa Utaratibu wa Kufuatilia**

- ☐ Upimaji wa viegezo na vipimo maalumu virasimiwe kwa kila aina ya hatari zinazohusika.
- ☐ Kuwepo kwa mipango na nyaraka za kufuatilia mitandao iliyoko na iliyokubaliwa na wataalamu na mamlaka husika.
- ☐ Vifaa vya kiufundi vinavyoweza kutumika katika maeneo ya kawaida na hali za kawaida, kuwekwa na wafanyakazi wafundishwe jinsi ya kutumia na kuvitunza.
- ☐ Takwimu na uchambuzi unaoweza kutumiwa kutoka mitandao ya kimaeneo, maeneo yanayokaribian na njia za kimataifa zinazopatikana.
- ☐ Takwimu kupokelewa, kutayarishwa na kupatikana katika miundo inayofaa na kupatikana katika wakati unaofaa au karibu na wakati unaofaa.
- ☐ Kuwa na mkakati wa kupata, kuchunguza na kusambaza takwimu za tishio la kuweza kuathiriwa na hatari.
- ☐ Takwimu zihifadhiwe kila mara na iweze kufikiwa kwa ajili ya kufanyiwa uthibitisho na matumizi ya utafiti.

**3. Kuanzishwa Taratibu za Utabiri na kutoa Hadhari**

- ☐ Uchambuzi wa takwimu, ubashiri na utoaji wa hadhari katika msingi wa njia za kisayansi na kiteknolojia zinazokubalika.
- ☐ Bidhaa za takwimu na hadhari zitolewe katika kiwango cha kimataifa na protokali.
- ☐ Wachambuzi wa hadhari kufundishwa katika kiwango cha kimataifa.
- ☐ Vituo vya kutoa hadhari kuwa na vifaa sahihi vinavyohitajika kutunza takwimu na pia kuendesha utabiri.
- ☐ Kuwa na mfumo unaofanya kazi wakati wote kama vile umeme wa akiba wakati unakatika, vifaa vya akiba na utaratibu wa kuwaita wafanyakazi kwa zamu.
- ☐ Hadhari kutolewa na kusambazwa kwa ufanisi, kwa wakati na katika mfumo unaolingana na mahitaji ya mtumiaji.
- ☐ Kuwa na mpango maalum wa kufuatilia na kutathmini utaratibu wa uendeshaji, ikiwa ni pamoja na ubora wa takwimu na utendaji wa hadhari.

*Kipengele Muhimu 3:* **USAMBAZAJI NA MAWASILIANO**

**Shabaha:** *Kuimarisha taratibu za mawasiliano na usambazaji ili kuhakikisha watu na jamii wanatahadharishwa mapema juu ya maafa yanayoweza kutokea na kuwezesha uratibu wa kitaifa au kimaeneo na kubadilishana taarifa.*

## Washiriki Muhimu

Mashirika ya Kimataifa, kitaifa na kimaeneo ya kukabiliana na maafa; Idara ya huduma za taifa za utabiri wa hali ya hewa na maji; Mamlaka za kijeshi na wanaharakati; Mashirika ya Vyombo vya Habari (k.m. magazeti, televisheni, radio na mitandandao); Wenye biashara katika maeneo yanayotishiwa kuathiriwa (k.m. utalii, nyumba za utunzi wa wakongwe, vyombo vya majini); Mashirika ya kimsingi ya kijamii na ya vijijini; Mashirika ya kimataifa na ya Umoja wa Mataifa kama vile UN/ISDR, IFRC, UNDP, UNESCO, UNEP, WMO, OCHA.

## Orodha ya Uhakiki

**1. Kuweka taasisi ya Mipango na Kutoa maamuzi**

- ☐ Usambazaji hadhari kuimarishwa kupitia sera za serikali au sheria (k.m. ujumbe kupitishwa na serikali hadi kwa wasimamizi wa mashirika na Jamii n.k.).
- ☐ Mamlaka zinazotambuliwa kwa ajili ya kusambaza ujumbe wa hadhari (k.m. mamlaka ya utabiri wa hali ya hewa kutoa ujumbe wa tahadhari za hali ya hewa, mamlaka ya Afya kutoa ujumbe wa tahadhari za Afya).
- ☐ Shughuli, Majukumu na uwajibikaji wa kila mhusika katika utaratibu wa kusambaza hadhari kama ilivyopasishwa na sheria au sera ya serikali (k.m. huduma za utabiri wa hali ya hewa na maji pamoja na mashirika yasiyo ya serikali NGOs).
- ☐ Kuelezwa majukumu na uwajibikaji wa kimaeneo au hadhari ya eneo lote, ikiwa ni pamoja na usambazaji wa hadhari hadi kwa nchi jirani.
- ☐ Mtandao wa watu wa kujitolea kufundishwa na kuwezeshwa jinsi ya kupokea na kusambaza ujumbe wa hadhari hadi vijijini na jamii.

**2. Usimikaji wa Taratibu nzuri za Mawasiliano na Vifaa**

- ☐ Taratibu za mawasiliano na usambazaji unaombatana na mahitaji ya jamii husika (k.m. Radio na Televisheni kwa wale wanaoweza kuzifikia; na ving'ora, vitambaa vya ilani au kuonya au watu wa kukimbiza ujumbe kwa Jamii ya sehemu za mashambani).
- ☐ Teknolojia ya mawasiliano ya kuonya inafikia watu wote, ikiwa ni pamoja na watu wanaosafiri au maeneo ya ndani.
- ☐ Kuwasiliana na mashirika ya kimataifa au wataalamu ili kusaidia na utambuzi pamoja na upatikanaji wa vifaa vinavyofaa.
- ☐ Matumizi ya Vyombo vya habari kwa jumla kwa usambazaji wa ujumbe (k.m. vyombo vya usambazaji habari visivyokuwa rasmi).
- ☐ Mikataba juu ya matumizi ya sekta binafsi inapowezekana(k.m. radio chipukizi, makazi salama).
- ☐ Mfululizo wa usambazaji wa hadhari na taratibu za mawasiliano kwa hali zote za hatari.
- ☐ Utaratibu wa mawasiliano ni wa pande zote mbili na kuingiliana ili kuruhusu uthibitisho wa kupokewa hadhari.
- ☐ Matengenezo ya vifaa na utekelezaji wa mpango wa kuimarisha na kuondoa vifaa vibovu ili kuwepo na vifaa vya dharura endapo kutakuwepo na kukwama.

**3. Ujumbe wa Hadhari Kutambuliwa na Kueleweka**

- ☐ Ujumbe wa hadhari unaoelekezwa kwa ajili ya mahitaji ya walioko hatarini (k.m. tamaduni tofauti, kijamii, kijinsia, lugha na misingi ya elimu).
- ☐ Tahadhari na ujumbe kulingana na maeneo ya kijiografia kuhakikisha hadhari inapelekwa kwa wale wanaotishiwa peke yao.
- ☐ Ujumbe ujumuishe ufahamu wa thamani, wasiwasi na maslahi ya wale watakaohitaji kuchukua hatua (k.m. maagizo ya kuwalinda mifugo na wanyama wa kufuga ndani).
- ☐ Ujumbe wa hadhari utambulike bayana na endelevu kwa muda mrefu inapohitajika.
- ☐ Hadhari ieleze wazi juu ya hali ya tishio na athari zake.
- ☐ Uwepo utaratibu wa kufahamisha jamii endapo tishio limekwisha.
- ☐ Uchunguzi wa jinsi watu wanavyotafsiri ujumbe wa hadhari unaotolewa na wanachojifunza, na kuwekwa katika mifumo ya ujumbe na taratibu za usambazaji.

*Kipengele Mihimu 4:* **UWEZO WA KUKABILI**

**Aim:** *Kuimarisha uwezo wa jamii wa kuitikia ujumbe wa maafa kupitia elimu ya hatari za maafa, ushiriki wa jamii na maandalizi ya kukabiliana na maafa.*

## Washiriki Muhimu

Mashirika ya kijamii ya sehemu za mashambani; shule. Vyuo vikuu; sekta ya elimu isiyokuwa rasmi, vyombo vya habari;(magazeti, radio na televisheni na mitandao); mashirika ya kiufundi yenye elimu ya kukabiliana na maafa, mashirika ya kukabiliana na maafa katika maeneo, mashirika ya kimataifa na ya Umoja wa mataifa kama vile OCHA, UNDP, UNEP, FAO, UNESCO, UN/ISDR, IFRC, WMO.

## Orodha ya Uhakiki

**1. Hadhari Kuheshimiwa**

- ☐ Hadhari zinazotayarishwa na kusambazwa kwa wale wanaotishiwa na hatari kufanywa na mashirika yanayoheshimika (k.m. Serikali, Viongozi wa kidini, mashirika ya kijamii).
- ☐ Maoni ya raia juu ya hatari za maafa ya kiasilia na huduma ya hadhari ichambuliwe ili kukadiria upokeaji wa jamii.
- ☐ Kuimarishwa mikakati ya kujenga heshima na kuaminiwa kwa hadhari (k.m. kuelewa tofauti ya utabiri na hadhari).
- ☐ Ujumbe wa udanganyifu upunguzwe kabisa na uimarishaji wake uelezwe ili kujenga imani katika utaratibu wa kutoa hadhari.

**2. Kuanzishwa mipango ya Maandalizi na kukabiliana na Maafa**

- ☐ Maandalizi ya kukabiliana na Maafa yanawezeshwa kisheria.
- ☐ Mipango ya maandalizi ya kukabiliana na maafa kwa kulenga mahitaji binafsi ya jamii zinazotishiwa kuathiriwa.
- ☐ Ramani za majanga na uwezekano wa kuathiriwa kutumiwa kuandaa mipnago ya kujiandaa na kukabiliana na maafa
- ☐ Mipango inayoenda na wakati ya kujiandaa na kukabiliana na dharura kuanzishwa, kusambaziwa kwa jamii na kutumiwa.
- ☐ Matukio ya maafa yaliyopita na jinsi yalivyoshughulikiwa kuchambuliwa na mafunzo yaliyopatikana kujumuishwa katika mipango ya kukabiliana na maafa.
- ☐ Mikakati itekelezwe kwa ajili ya kudumisha hali ya kuwa tayari kwa marejeo ya maafa.
- ☐ Majaribio ya mara kwa mara na mazoezi kufanywa ili kupima uwezo taratibu na usamabazaji wa hadhari.

**3. Kuhakikiwa na Kuimarishwa kwa Uwezo wa Mwitikio**

- ☐ Uwezo wa jamii kuitikia hadhari kikamilifu kufanyiwa uchambuzi
- ☐ Matukio ya maafa yaliyopita na jinsi yalivyopokewa kuchambuliwa, na mafunzo yaliyopatikana kujumuishwa katika mipango ya baadaye ya kukabiliana na maafa.
- ☐ Mashirika yanayofadhili mipango ya Kijamii yajumuishwe ili yasaidie na kazi ya ujenzi wa uwezo.
- ☐ Elimu ya Jamii na Watu wa kujitolea pamoja na mipango ya mafunzo iimarishwe na kutekelezwa.

**4. Kutolewa na Kuimarishwa kwa Elimu ya Umma**

- ☐ Maelezo ya kawaida juu ya maafa, uwezekano wa kuathirika, hatari na namna ya kupunguza athari za maafa kusambazwa kwa jamii iliyo katika uwezekano wa kuathiriwa.
- ☐ Elimu kwa jamii kuhusu namna hadhari zitakavyosambazwa na njia ya uhakika inayoweza kuwafikia na namna ya kuitikia kwa majanga tofauti baada ya ujumbe wa hadhari kupokelewa.
- ☐ Jamii kufundishwa namna ya kutambua ishara za kawaida za kutambua majanga yanayohusiana na hali ya hewa na maji kwa ajili ya kuruhusu mwitikio wa haraka.
- ☐ Matangazo ya mara kwa mara na elimu kuingizwa katika mitaala ya shule kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu.
- ☐ Matumizi ya vyombo vya habari na nyimbo au njia nyingine za mawasiliano ili kuongeza ufahamu wa raia.
- ☐ Ufahamu wa raia na kampeni za elimu kwa kulenga mahitaji ya kila mmoja (k.m. watoto; meneja wa maswala ya dharura na vyombo vya habari).
- ☐ Mikakati ya ufahamu wa raia na miradi kufanyiwa marekebisho angalau mara moja kwa mwaka na kuongezewa habari mpya inapohitajika.

*Maswala Nyeti zaidi:* **UONGOZI NA MIPANGILIO YA KITAASISI**

**Shabaha:** ***Kuanzisha Mfumo wa Kitaasisi, Kisheria na Sera utakaosaidia katika*** *utekelezaji na udumishaji wa taratibu bora za hadhari.*

## Washiriki Muhimu

Viongozi wa kisiasa; viongozi wa serikali (k.m. idara za mazingira, maendeleo na mipango); mashirika ya kukabiliana na maafa ya Kimataifa, kitaifa na katika maeneo; mashirika ya utabiri wa hali ya hewa na maji; mashirika mengine ya kimataifa na mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile UNDP, UNEP, FAO, UNESCO, UN/ISDR, WMO, Benki ya dunia benki za maendeleo za kimaeneo RC.

## Orodha ya Uhakiki

**1 Hadhari kupewa kipaumbele kimataifa na Kimaeneo**

- ☐ Manufaa ya kiuchumi ya hadhari kufahamishwa viongozi wa vyeo vya juu serikalini na Viongozi wa kisiasa, kwa njia ambazo hazina gharama sana kama vile uchambuzi wa gharama kwa miradi ya maafa iliyopita.
- ☐ Mifano ya uchunguzi wa taratibu za hadhari zitawanywe kwa viongozi wa serikali na viongozi wa kisiasa.
- ☐ Mabingwa wa shughuli za hadhari watumiwe kwa kutangaza hadhari na manufaa yake.
- ☐ Kutambuliwa eneo la hatari linalopasa kupewa kipaumbele na kuanzishwa mipango ya utekelezaji kupitia mfumo wa njia nyingi za kukabiliana na maafa.
- ☐ Hadhari kujumuishwa katika mpango wa Uchumi wa taifa.

**2. Kuanzishwa mifumo ya Sheria na Sera ili Kuwezesha Hadhari Kutekelezwa**

- ☐ Sheria au sera ya Taifa kuimarishwa kwa ajili ya kutoa misingi ya kitaasisi na kisheria kwa utekelezaji wa taratibu za hadhari.
- ☐ Kufafanuliwa majukumu na uwajibikaji kwa mashirika yote (ya serikali na yasiyo ya serikali) yanayoshiriki katika hadhari.
- ☐ Jukumu la pamoja na mamlaka ya kushirikisha hadhari na kukabidhiwa shirika moja la taifa.
- ☐ Kiongozi mmoja wa kisiasa au ofisa mkuu wa serikali anayekubaliwa kisheria kama mtoaji maamuzi ya taifa.
- ☐ Kuimarishwa sera ya kutawanya shughuli za usimamizi wa maafa na kuhimiza ushiriki wa jamii.
- ☐ Utoaji maamuzi mashinani na utekelezaji wa taratibu hadhari uliowekwa kukidhi uasimamizi mkubwa zaidi na uwezo wa nafasi katika kiwango cha taifa au kimaeneo.
- ☐ Mikataba ya kimaeneo na mipakani iliyobuniwa kwa kuhakikisha taratibu za hadhari zinajumuishwa inapowezekana.
- ☐ Uhusiano na ushirikiano kati ya mashirika yote yanayohusika na hadhari kuwekwa katika taasisi moja na kushirikishwa.
- ☐ Hadhari hujumuishwa katika upunguzaji maafa na sera za maendeleo.
- ☐ Utaratibu wa ufuatiliaji na mamlaka utekelezaji ianzishwe kusaidia sera na sheria.

**3. Uwezo wa Taasisi Kuhakikiwa na Kuimarishwa**

- ☐ Uwezo wa Mashirika yote na taasisi zote kuhakikiwa na mipango ya kuimarisha na mipango ya mafunzo kuendelezwa na kuwezeshwa.
- ☐ Sekta ya mashirika yasiyo ya serikali kuingizwa na kuhimizwa kuchangia juhudi za kuimarisha uwezo.

**4. Kupatikana Uwezo wa Fedha**

- ☐ Utaratibu wa ufadhili wa fedha kutoka serikalini kwa maandalizi ya kukabiliana na hadhari na maafa kuendelezwa na kufanywa kuwa taasisi.
- ☐ Utafutaji wa misaada ya fedha katika ngazi ya kimataifa au kimaeneo.Ushiriki wa watu wote/binafsi kutumiwa kwa kusaidia uimarishaji wa taratibu za hadhari.

# ORODHA YA MIFUPISHO

| | |
|---|---|
| EWC III | Mkutano wa III wa Kimataifa juu ya Onyo la Awali. |
| FAO | Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. |
| IFRC | Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu |
| ITU | Shirika la Kimataifa la Mawasiliano ya Simu |
| NGO | Mashirika Yasiyo ya Serikali |
| OCHA | Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa ya Ushirikishi wa Misaada ya Kibinadamu |
| PPEW | Jukwaa la Utangazaji wa Onyo la Awali |
| UN | Umoja wa Mataifa |
| UNDP | Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| UNEP | Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa |
| UNESCO | Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| UN/ISDR | Shirika la Umoja wa Mataifa la Mikakati ya Kimataifa ya Kukabiliana na Maafa |
| UNOSAT | Mpango wa Umoja wa Mataifa wa kuipa Jamii ya Kibinadamu nafasi ya Huduma za Maelezo ya Picha na Jiografia kwa njia ya Satelait. |
| UNU-EHS | Taasisi ya Chuo Kikuu cha Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira na Ulinzi wa Binadamu. |
| WMO | Shirika la Utabiri wa hali ya hewa Duniani |

## Maelezo ya Mawasiliano

**UN/ISDR Platform for the Promotion of Early Warning (PPEW)**
Hermann-Ehlers-Strasse 10
D - 53113 Bonn
Germany
isdr-ppew@un.org
www.unisdr-earlywarning.org

**UN Secretariat of the International Strategy for Disaster Reduction (UN/ISDR)**
Palais des Nations
CH - 1211 Geneva 10
Switzerland
isdr@un.org
www.unisdr.org

*Nyaraka hii imetokana na Mkutano wa Tatu wa Kimataifa juu ya Onyo la Awali (EWC III) ulioandaliwa na serikali ya Ujerumani chini ya Umoja wa Mataifa , kutoka tarehe 27 hadi 29 Machi 2006 huko mjini Bonn, Ujerumani.*